**Noa Bongo Jenga Maisha Yako !**

**Utandawazi : Watumishi wa Kike Burundi**

**Autorin : Justine Bitagoye**
**Redaktion ; Yann Durand**
**Übersetzung ; Anne Thomas**

---

**3 Stimmen ……………..Sauti 3**
- **junger Spreche 1 ……………Msimulizi wa kiume 1**
- **junge Sprescherin …………..Msimulizi wa kike 1**
- **Sprescher(in) 2………………Msimulizi wa kike 2**

**als Off – Stimme für die Reportage**

---

**Vorspann LbE…………………..Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA KWANZA REPORTAGE : REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1 :**

Habari gani!Natumai nyote hamjambo !

**Msimulizi wa kiume 1 :**

Leo katika mfululizo wa vipindi vyetu juu ya utandawazi tutazungumzia kuhusu umaskini ambao unaviacha vijiji kuwa vitupu…….

**Msimulizi wa kike 1 :**

………..ni kuhusu umma kuvikimbia vijiji.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Miongoni mwa watu wanaokimbilia mijini wengi wao ni vijana na wengi zaidi ni wasichana ambao huajiriwa kama watumishi wa nyumbani.

**Msimulizi wa kike 1 :** Tutamtembelea mmojawapo wa watumishi hao wa nyumbani.

**Msimulizi wa kiume 1 :**…na tunaelekea Bujumbura mji mkuu wa Burundi.

**Msimulizi wa kiume 1 na Msimulizi wa kike 1 :**

Kwa hiyo fungeni mikanda yenu tayari kwa safari !

**………..Manuscript …………………………..**

**Globalisierung Hausdiens Atmo 1 …………………………**

**Msimulizi wa kike 2 :** Jeannine ana miaka 17.Anatoka Muyinga kaskazini mwa Burundi Jeannine aliacha shule alipokuwa na umri wa miaka 11.Alikuwa hajuwi kusoma wala kuandika.Wakati alipokuwa na umri wa miaka 16 aliiacha familia yake na kijiji chake kwenda kujaribu bahati yake mjini,

**Globalisierung Hausdienerinnen 1**

Nimeamua kuja mjini Bujumbura kwa sababu nilikuwa maskini mno nilikuwa na nguo moja tu.Wazazi wangu walikuwa hawawezi kunisaidia na tulikuwa hatuna pesa.Na baya zaidi pale wakati ninapowaona marafiki zangu wakirudi kijijini kutoka mjini walikuwa wananivutia mno.Walikuwa wakivalia vizuri sana na nilikuwa nawaonea wivu.Niliondoka bila ya kuwaeleza wazazi wangu.Rafiki yangu mmoja alinisaidia kupata familia moja ambayo ningeliweza kuifanyia kazi.Bosi wangu alikuwa akiishi katika kitongoji cha Bujumbura kinachoitwa Kanvosha, Ni kitongoji cha kimaskini ambapo watu wengi walikuwa ni wakimbizi wa vita.

**Globalisierung Hausdien Atmo 2**

Kazi yake ya kwanza takriban ilikuwa kama mateso.

**Globalisierung Hausdienerinnen 2 ……………………..**

Asubuhi na mapema inabidi nikachote maji kutoka kisimani kuanzia saa kumi na mbili hadi saa mbili na halafu inabidi nipike.Na saa tano inabidi nisafishe nyumba.Wakati wa mchana nilikuwa nikiruhusiwa kulala kwa kama saa moja hivi. Halafu mkuu wangu bwana mwenye nyumba hunituma kazi nyengine kama vile kwenda kufanya manunuzi.Nilikuwa nikichoka na nilikuwa na huzuni.
Kutokana na kuchoshwa na kazi zisizokuwa na mapumziko. Jeannine aliamuwa kuondoka.Kwa haraka alifanikiwa kupata muajiri mpya na kazi yake ikawa ni kumuangalia mvulana wa miaka 3.

**Globalisierung Hausdien Atmo 3**

Ilikuwa ikibidi achote maji kutoka kisimani asubuhi na mapema, atayarishe chakula cha asubuhi na kumpeleka mtoto shule. Halafu akiosha vyombo,akisafisha nyumba,akenda sokoni, akipika,akifua halikadhalika akipiga pasi …kazi zote hizo kwa
malipo ya faranga 12,000 za Burundi kwa mwezi sawa na euro 6.90 za Ulaya.

**Msimulizi wa kike 1 :** Kimsingi ilikuwa afanye kila kitu kwa pesa kidogo sana.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Lakini wakati gani anapumzika ?

**Msimulizi wa kike 2:** Muajiri wake mtumishi wa kike huyo yaani mama mwenye  nyumba alikuwa ameweka wazi kwamba Jeannine anapata masaa mawili ya kupumzika kwa siku……. wakati wa mchana.

**Globalirisierung Hausdienerinnen 3**

Nafikiri faranga 12,000 zinatosha kwa sababu huwa namuangalia kwa mambo mengine yote yale.Serikali hailipi kitu cha maana.Mtumishi wa serikali kwa wastani hulipwa kama faranga 60,000 haipindukii 70,000.Kwa hiyo sisi hatuwezi kupindukia kiwango hicho.

**Globalirisierung Hausdien Atmo 4**

**Msimulizi wa kike 2 :** Licha ya kuwa anachoka.Jeannine daima huwa anatabasamu.

**Globalisierung Hausdienerinnen 4**

Katika kipindi cha usoni ningelipenda kuanzisha biashara ndogo.Nahitaji faranga 500,000 za Burundi (sawa na euro 290) kuanzisha biashara hiyo.Lakini ni vigumu kukusanya pesa hizo zote.Kwa hivi sasa nina faranga 20,000 tu (sawa na euro 116)

**Msimulizi wa kike 2 :** Jeannine hajutii uamuzi wake wa kuja mjini.Mara mbili kwa mwaka huwa anarudi kijijini kuiona familia yake.Anajihisi kutukuka kwa kulinganishwa na kaka zake na dada zake wanaoendelea kubakia kijijini.Daima huwa anawapelekea zawadi na anafurahia safari hiyo licha ya kwamba humgharimu mshahara wake wa miezi sita.

**Globalisierung Hausdien Atmo 5 dann runter (im O-Ton 5 wieder hoch)…………………………………………..**

Bujumbura imejaa watumishi wa kike wa nyumbani wenye majaaliwa kama yale ya Jeannine.Hawana mikataba ya kazi na waajiri wao wanaweza kuwaonea na wasiwe na la kufanya.. Goreth Kanyange ni rais wa TWESE TWOTERIMBERE ikimaanisha maendeleo kwa kila mtu ambalo ni shirika la watumishi wa majumbani.

**Globalisierung Hausdienerinnen 5**

Shirima letu huwafunza watumishi wa kike wa majumbani jinsi ya kusoma na kuandika.Na juu ya hilo hujifunza Kingereza na Kifaransa ili waweze pia kufanya kazi kwa wageni. Hujifunza juu ya usafishaji,kupiga pasi,kupika,kutengeneza bustani na pia kuhusu taratibu za itifaki.Kimsingi kila kile wanachotakiwa kukijuwa iwapo waajiriwa wao wanapokuwa hawapo.

**Atmo 5 wieder hoch und runter O-Ton 5 geht dann weiter ………………………………….**

Wazo la kuanzisha shirika hili lilikuja baada ya kuona mizozo kati ya watumishi wa nyumbani na waajiri wao. Tuligumduwa kwamba kwa kadri wanapofanya kazi vizuri ndipo wanapolipwa vizuiri zaidi.Hilo ndio lengo la shirika letu.

**Globlisierung Hausdien Atmo 6……………………**

**Globalisierung Hausdienerinnen 6……………………………..**

Leo tumejifunza namna ya kutengeneza saladi na kupika keki. Faida ya kuwa kwenye shirika hili ni kwamba unapata mshahara mzuri.Muajiri anajuwa kwamba unaweza kufanya kazi yako kwa sababu ya ujuzi ulioupata hapa.Kabla ya kujiunga na shirika hili nilikuwa nikipata faranga 15,000 (sawa na euro 8.7 ) lakini sasa napata faranga 25,000 (sawa na euro 14.5) Jeannine kwa upande wake bado ana safari refu kuweza kufikia kipato anacholipwa Cassilde cha faranga 25,000.Safari ndefu kuweza kufikia mshahara huo na safari ndefu ya kuweza kufanikisha ndoto yake ya kuwa na familia yake mwenyewe.

**Globalisierung Hausdienerinnen 7…………………**

Bila ya shaka ninata kuwa na …..Mimi ni mwanamke na inabidi niwe na watoto.Hiyo ni ndoto ya kila mtu mwanaume au mwanamke.

**Globalisierung Hausdien Atmo 7 …………**

Licha ya matatizo anayokabiliana nayo katika maisha yake ya kila siku Jeannine hayuko tayari kurudi tena kijijini kwa vile ameweza kupata kazi na hakuishia kuwa mzururaji kama vile walivyo watu wengi katika miji mikuu ya Afrika.Amekipa kisogo kijiji chake milele.

**MWISHO WA SEHEMU YA KWANZA**

## SEHEMU YA PILI …….. ERKLÄRSTÜCK

**Msimulizi wa kiume 1 na Msimulizi wa kike 1 tu !**

**Msimulizi wa kiume :** Katika ile repoti Jeannine alikuwa na umri wa miaka 17 tu! Ni umri mdogo kwa kulinganishwa na kazi nyingi alizokuwa akifanya au sivyo?

**Msimulizi wa kike :** Inategemea!Kwa mujibu wa Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Mtoto anahesabika kuwa mototo kwa sababu hakutimia umri wa miaka 18 na anapaswa kulindwa dhidi ya unyonyaji wa kiuchumi.

**Msimulizi wa kiume :** Kwa hiyo ina maana hapo hatakiwi kufanya kazi…….

**Msimulizi wa kike :** Tafsiri yake haiwi rahisi hivyo.Kifungu nambari 32 kinazungumzia juu ya kazi yumkini ikawa ya hatari au ina madhara kwa motto.

**Msimulizi wa kiume :** Lakini makubaliano hayo uliyoyataja ni nini hasa ?

**Msimulizi wa kike :** Ni aina ya mkataba uliotayarishwa na Umoja wa Mataifa. Una kanuni za aina mbali mbali kuhakikishwa kwamba watoto wanalindwa.Kwa ujumla una vifungu 52.

**Msimulizi wa kiume :** Na dunia yote kweli inazingatia sheria hizo?

**Msimulizi wa kike :** Kati ya nchi 195 nchi mbili bado hazikuridhia mkataba huo …Marekani kwa sababu bado wanatekeleza hukumu ya adhabu ya kifo na hawataki kuifuta katika majimbo yake fulani.Nchi nyengine ni Somalia kutokana na serikali yake bado kutotambuliwa na Umoja wa Mataifa.

**Msimulizi wa kiume :** Kwa hiyo inaonekana hata zile nchi zilizosaini bado hazitekelezi kwa ukamilifu makubaliano hayo…….

**Msimulizi wa kike :** Siku zote kunakuwa na tafauti kubwa kati ya nadharia na vitendo na juu ya hilo kila nchi huruhusiwa kukikataa kifungu hiki au kile iwapo haikiendani na sheria yake ya taifa.

**Msimulizi wa kiume :** Kuna mfumo wowote ule wa kufuatilia utekelezaji wake ?

**Msimulizi wa kike :** Ndio upo….kuna shirika yaani Kamati ya Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Mtoto ambayo inatakiwa ihakikishe kwamba mkataba huo unatekelezwa.Kila baada ya miaka mitano kila nchi huandaa repoti juu ya hatua ilizopitisha ili kutimiza ahadi zake za mkataba.

**Msimulizi wa kiume :** Lakini angalau katika  kesi fulani watoto waliokandamizwa wanaweza kjitetea wenyewe!

**Msimulizi wa kike :** Ndio ni kweli lakini kuna wengine wengi idadi yao isiohesabika ambao hawana la kufanya kuweza kujitetea.Takriban watoto milioni 1.2 duniani kote wanafanya kazi kwenye mazingira yanayokiuka Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Mtoto.

**Outro……Funga Kipindi……**

**Msimulizi wa kike 2 :**
Na hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha Noa Bongo-Jenga Maisha Yako!. Asante kwa kusikiliza kipindi hiki juu ya utandawazi kuhusu kukimbiwa kwa vijiji na umma na utumikishaji wa watoto.Ni kipindi cha Deutsche Welle kilichotayarishwa na Justine Bitagboye na Yann Durand. Ili kujuwa zaidi au ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki tafadhali nenda kwenye tovuti yetu www.de-world.de/be
Usikose kuwa nasi tena mara nyengine!
Kwaheri !